

Mfumo dume wahusishwa na matokeo ya ufisadi

Na Yusuph Mussa, Lushoto

BAADHI ya wadau wamesema kushamiri kwa ufisadi nchini ni matokeo ya mfumo dume kwa vile ofisi nyingi ikiwemo zile za Serikali na binafsi

kujaa wanaume, lakini kama wanawake watapewa nafasi zaidi na kuwa asilimia 50 kwa 50 katika nyanja mbalimbali rushwa itapungua kama sio kwisha kabisa.

Hayo yalisemwa hivi karibuni kwenye mdahalo wa Usawa wa Jinsia uliofanyika Kijiji cha Mwangoi, Jimbo la Mlalo wilayani Lushoto Mkoa wa Tanga na kuwashirikisha viongozi wa dini, vyama vya siasa, vijiji wakiwemo watendaji na wenyeviti wa vijiji na wananchi.

Akitoa mada, mwezeshaji Sophia Mwakagenda alisema mfumo dume bado ni tatizo nchini na jamii inatakiwa kubadilika na kutoa fursa sawa kwa wote ikiwemo wanawake kushika nafasi mbalimbali na kusema hata rushwa ipo kwa vile wanaume ndiyo wameshika nafasi za juu.

Ufisadi umeshamiri kwenye ofisi mbalimbali nchini ikiwemo za Serikali na sekta binafsi kwa vile wenye mamlaka wengi ni wanaume, lakini kama wanawake wangepewa nafasi hizo ufisadi usingekuwepo," alisema Mwakagenda.

Mwakagenda alisema, wanawake waliokwenda kwenye Mkutano wa Beijing walikuja na mtazamo hasi kiasi cha kuleta mtafaruku kwenye jamii kwani walidhani wamekuja kupora haki za wanaume, kumbe wamekuja kujenga hoja ili zile mila na desturi kandamizi kwa watoto wa kike ziondolewe.

Tunasikitika, wanawake tangu watoke Beijing hawajaweza kuibadilisha jamii, kwani walikuja na mtazamo hasi kuwa wanakuja kuwakomoa wanaume na badala yake ule mfarakano hata kwa upande wa viongozi wa dini.

Nia ya kuwakutanisha wanawake kule ilikuwa ni njema na hilo nchini za Scandinavia kama Denmark, Norway na Finland wamefanikiwa. Ni kutaka wanawake hasa watoto wa kike wapewe

fursa ikiwemo elimu na kuondolewa kwa mila na desturi kandamizi kama urithi na shughuli za kijamii.

Mwakagenda aliwataka wanaume kuwapa fursa sawa wake zao za kujiingizia kipato, kama mke amekopa fedha kwenye SACCOS afanye jitihada kuona mke anarudisha mkopo huo, sio kuchukua fedha hizo na kwenda kunywa pombe ama kuhonga wanawake wengine.

Mwezeshaji mwingine, Kiama Mwaimu alisema hawana ugomvi na mambo ya asili kati ya mwanamke na mwanaume, bali ugomvi wao ni kuona mwanamke anapewa fursa ya kutoa ushauri na maamuzi baada ya kujadili kwa pamoja kati ya mke na mume.

Hatuna ugomvi na mama kuzaa, hilo ni jambo la asiliya maumbile, lakini ugomvi wetu ni usawa wa kazi, ushirikiano katika kutoa maamuzi na maendeleo ya kweli ndani ya nyumba yatapatikana iwapo mke na mume watashirikiana, historia inaonesha hivyo.